BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 27 Novemba, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 03 Oktoba, 2024.

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Kazi za Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Taarifa ya Nane ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Taarifa ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi juu ya Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Kazi za Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora juu ya Taarifa ya Nane ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

95. MHESHIMWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Siku ya maafa duniani ni siku muhimu sana kwa jamii na taifa kwa ujumla yenye lengo la kuikumbusha jamii jinsi ya kukabiliana na majanga yakiwemo yale ya kimaumbile na ya kibinaadamu.

    (a) Je, ni kwa jinsi gani viongozi wa shehia wanashirikishwa katika kukabiliana na maafa katika jamii zao.

    (b) Je, ni yepi hasa majukumu ya Kituo cha Kukabiliana na Maafa kilichopo Kidongochekundu.

    (c) Je, uelewa wa wananchi uko vipi juu ya kituo hiki.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

1. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

    (a) Kwa kiasi gani jamii ya watu wenye ualbino Zanzibar inalindwa dhidi ya dhana potofu juu yao.

    (b) Kwa kiasi gani Wizara yako ikishirikiana na jamii, inatoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya kupata uelewa mzuri kutokana na dhana hiyo potofu.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

84. MHESHIMIWA CHUM KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naendelea kutoa pongezi zangu kwa Wakala wa Ulinzi (JKU) kwa kutoa huduma ya ulinzi katika taasisi mbali mbali. Hata hivyo, kuna taarifa kuwa watendaji wa Wakala hii hawalipwi malipo yao ingawa taasisi inayopewa huduma ya ulinzi hulipa malipo yote yanayotakiwa.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea watendaji hao kutokulipwa fedha zao kwa wakati.

(b) Ni ipi ahadi ya Serikali juu ya ulipwaji wa malipo hayo.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

102. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, Serikali iliandaa utaratibu wa wananchi kuweza kupata mikopo, pamoja na ukweli kuwa wananchi wengi bado hawajapata mikopo hiyo.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuwepo kwa changamoto hiyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

105. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taarifa zinaonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la watumiaji wa huduma za mawasiliano ya data na sauti pamoja na ongezeko la miamala ya fedha kwa kutumia simu za mkononi na mtandao (internet) hapa nchini. Pamoja na ongezeko hilo bado mgawanyo wa mapato baina ya pande mbili za Muungano (Zanzibar na Tanzania bara) haujawekwa wazi.

(a) Je, ni upi mgawanyo wa mapato ya tozo za miamala ya simu kisheria kwa Zanzibar na Tanzania bara.

(b) Je, ni kanuni na sheria ipi inayosimamia miamala ya simu baina ya Zanzibar na Tanzania bara.

(c) Je, ni upi mnyumbuliko wa matumizi ya fedha zilizokusanywa kwenye miamala ya simu.

119. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Zanzibar imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizo kumekuwepo na malalamiko kuhusu kukosekana kwa muunganiko wa kodi hali inayosababisha utitiri wa kodi kwa wawekezaji hao.

(a) Je, ni aina gani za kodi ambazo mwekezaji anapaswa kulipa ili aweze kuwekeza Zanzibar.

(b) Je, ni misamaha gani ya kodi ambayo mwekezaji anaweza kuipata kutoka Serikalini anapowekeza Zanzibar.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

43. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa miaka mingi mfumo wetu wa elimu uliwaandaa wahitimu kuweza kuajiriwa.

(a) Je, kwa vipi na kwa mikakati ipi mahususi mfumo mpya wa elimu utawawezesha wahitimu kujiajiri.

(b) Kwa kupitia mfumo mpya wa elimu, je, mhitimu atakuwa na uwezo wa kujiajiri bila ya hofu yoyote katika ngazi gani ya elimu.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

30. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Sekta ya michezo kwa kiasi fulani imekumbana na vitendo vya udhalilishaji hususani kwa upande wa watoto.

(a) Je, Wizara yako inachukua jitihada zipi katika kukomesha vitendo kama hivi kwa watoto.

(b) Ni hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa makocha na viongozi mbali mbali waliohusika kuwadhalilisha watoto kwenye tasnia ya michezo.

80. MHESHIMIWA CHUM KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kutokana na kukuwa kwa lugha ya kiswahili kitaifa na kimataifa.

Je, ni sababu zipi zinazokwamisha kutokutumika kwa lugha hii katika sekta mbali mbali za kibiashara ili kukuza pato la nchi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

72. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kutokana na kukuwa kwa miji, ni lini Serikali itaanzisha ruti ya njia ya Fuoni Uwanja wa Ndege na Mwera Uwanja wa Ndege, ili kuwaondolea wananchi usumbufu.

76. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachukua juhudi kubwa katika kupunguza ajali za vyombo vya baharini.

(a) Je, Wizara yako imefanya tathmini ipi ya mafanikio na changamoto zinazoukabili usafiri wa vyombo vya baharini.

(b) Kuna mipango ipi ya utayari na uharaka katika kukabiliana na ajali za vyombo vya baharini.

**Wizara ya Afya:**

20. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Kuna tofauti ipi baina ya tiba mbadala na tiba asilia.

(b) Ni asilimia ngapi mpaka sasa ya wananchi wanaithamini tiba mbadala kwamba inaweza kuokoa maisha yao kwa kiwango kikubwa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

12. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Pamoja na Zanzibar kufahamika kama ni kisiwa cha viungo (Spice Island), kuna wasi wasi kuwa, mahitaji ya nje ya soko la viungo ni makubwa kuliko uwezo wa ndani wa kuzalisha.

(a) Je, ni semina, warsha na makongamano mangapi ambayo Wizara imefanya katika kuhamasisha na kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa wingi mazao ya viungo hapa nchini.

(b) Tathmini iko vipi juu ya wastani wa uzalishaji wa ndani wa mazao ya viungo kwa sasa.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto :**

109. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la vituo vya kulelea watoto mayatima vya watu binafsi katika maeneo ya Zanzibar. Pamoja na vituo hivi kupata usajili kutoka Wizara husika, kumekuwa na malalamiko ya kuendeshwa vituo hivyo kinyume na sheria.

(a) Je, kuna vituo vingapi vya watu binafsi vya kulelea mayatima Zanzibar ambavyo vimepata usajili.

(b) Je, ni upi muongozo wa uendeshaji wa vituo vinavyotoa huduma ya malezi kwa watoto mayatima Zanzibar.

(c) Je, ni kwa namna gani jamii inawasaidia watoto mayatima hasa wale wanaolelewa katika vituo vya kulelea watoto Zanzibar ili kuinua ustawi wao.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

117. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi:

Pamoja na juhudi za Serikali za kukabiliana na utumiaji wa zana haramu, kumekuwepo na ongezeko la uvuvi haramu, ikiwemo matumizi ya nyavu zilizopigwa marufuku ambazo husababisha uharibifu mkubwa wa mazalio ya samaki.

(a) Je, tathmini iko vipi juu ya matumizi ya zana zisizoruhusiwa katika uvuvi hapa Zanzibar.

(b) Je, Serikali inashughulikia vipi suala la uingizaji wa zana haramu za uvuvi ikiwa ni pamoja na nyavu zenye macho madogo.

(c) Je, ni mkakati upi wa muda mrefu wa Serikali wa kuondoa kabisa tatizo la utumiaji wa zana haramu za uvuvi Zanzibar.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

55. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Kwa nini ujenzi na ukarabati wa jengo la Beitul Ajaib linachukua muda mrefu sasa.

(b) Kwa sasa hatua za ujenzi zimefikia asilimia ngapi.

(c) Tathmini iko vipi juu ya uhifadhi wa malikale zilizokuwemo ndani ya jengo hilo baada ya kuporomoka kwake.

## IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

### Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Taarifa ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Kazi za Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa mwaka 2023/2024

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Taarifa ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Taarifa ya Nane ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka 2023/2024

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**27 Novemba, 2024.** **KATIBU WA BARAZA.**